



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**



**MPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI KWA MWAKA 2024/2025**

Mpango na bajeti ya mwaka 2024/2025 imeandaliwa kwa kuzingatia mambo muhimu kama ifuatavyo: -

- Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025.
- Dira ya maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025.
- Maelekezo na ahadi mbalimbali za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.
- Malengo Endelevu ya Maendeleo 2030.
- Halmashauri imejikita katika miradi inayolenga kuleta matokeo chanya na yenye kugusa maisha ya wananchi moja kwa moja.
- Mpango na bajeti ya Halmashauri umezingatia masuala ya mtambuka kama vile ushirikishwaji wananchi na wadau katika masuala ya Jinsia, mazingira, vijana, ukimwi na kuzuia rushwa.
- Mpango wa lishe Kitaifa (Nutrition Programme)
- Mpango wa kitaifa wa kuzuia ukatili kwa wanawake na watoto (Social protection).
- Kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu.
- Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa asilimia 40 ya mapato inatengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**VIPUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025**

Halmashauri ya wilaya ya Magu kwa mwaka 2024/2025 imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

1. Kuanzisha na kuendeleza miradi ya kimkakati kwa ajili ya kuongeza mapato ya Halmashauri kwa: -
  - Kuendeleza ujenzi wa stendi ya kisasa ya Wilaya eneo la Ilungu
  - Kutwaa maeneo kwa ajili ya uwekezaji
  - Ujenzi wa vibanda 15 vya soko kuu
2. Kuboresha huduma za Afya kwa: -
  - Kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Afya Nyanguge.
  - Ununuzi wa vifaa tiba.

3. Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunza kwa:
  - Kukamilisha vyumba vya madarasa 27, ujenzi wa madarasa 32, nyumba 3 za walimu, matundu ya vyoo 125, ofisi 3 za walimu na kutengeneza madawati 3,904 katika shule za msingi. Ukamilishaji wa vyumba madarasa 21, ukamilishaji wa vyumba vya maabara 15, ofisi 4 za walimu na utengenezaji wa viti na meza 840 na ukamilishaji wa daharia 1 katika shule za Sekondari
  
4. Kuongeza ufanisi na utendaji wa kazi kwa: -
  - Kupunguza uhaba wa watumishi kwa kuajiri watumishi wapya 1495 kwa kada za Afya 129, Elimu Msingi 1008, Elimu Sekondari 278, Mifugo na uvuvi 3, Biashara 6, Maendeleo ya Jamii 8, Sheria 2, Tehama 1, Ukaguzi wa ndani 1, Ujenzi 2 na Utawala 57. Uhaba huu wa watumishi umetokana na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma kama vile Shule na Zahanati na watumishi wengine kustaafu Utumishi wa
  
5. Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi:
  - Kukamilisha ujenzi wa jengo la Halmashauri
  - Kukamilisha ujenzi wa Ofisi 1 ya Mtendaji wa kata na Ofisi 1 ya Mtendaji wa Kijiji

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Magu imeidhinishiwa jumla ya Tsh. **56,931,144,075.00** kutoka vyanzo vyake mbalimbali na kutoka ruzuku ya Serikali Kuu kama ifuatavyo: -

**MUHTASARI WA MAKISIO YA MAPATO KWA MWAKA 2024/2025**

<b>Na</b>	<b>Chanzo cha fedha</b>	<b>Makisio 2024/2025</b>
1	Mapato ya ndani	4,730,527,000.00
2	Ruuzuku ya miradi ya matumizi mengineyo	2,338,235,000.00
3	Ruzuku ya Mishahara	38,631,286,000.00
4	Miradi ya maendeleo –Ruzuku ya Serikali kuu	5,473,962,000.00
5	Miradi ya maendeleo- Fedha za Wahisani	5,757,134,075.00
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>56,931,144,075.00</b>

Naomba kuwasilisha.

Mohamed Ramadhani  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**MAGU**

**MUHTASARI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

<b>NA</b>	<b>JINA LA MRADI</b>	<b>BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2024/2025</b>
	<b>MIRADI YA FEDHA NDANI</b>	
1.	Miradi ya fedha za mapato ya Ndani	1,492,740,064.00
2.	Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo	84,176,000.00
3.	Ujenzi wa jengo la Halmashauri	700,000,000.00
4.	Ukamilishaji wa miundombinu ya elimu na afya	450,000,000.00
5.	Fedha elimu bila malipo- elimu awali na msingi	1,667,908,424.00
6.	Fedha elimu bila malipo – Elimu Sekondari	2,855,049,651.00
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>7,249,874,139.00</b>
	<b>MIRADI YA FEDHA WAHISANI</b>	
1	Mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi	480,339,000.00
2	Mradi wa kunusuru kaya maskini-TASAF	1,277,500,000.00
3	Mfuko wa Pamoja wa Afya –kuboresha huduma za afya (HBF)	759,570,000.00
4	Mradi wa uboreshaji miundombinu ya maji na usafi katika vituo vya kutolea huduma za afya. (RWSS	870,200,000.00
5	Mradi wa uboreshaji miundombinu ya maji na usafi katika vituo vya kutolea huduma za elimu. (SWASH)	294,167,000.00
6	Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu Elimu Msingi (BOOST)	1,020,758,000.00
7	Mradi wa uboreshaji miundombinu ya elimu sekondari (SEQUIP)	624,287,000.00
8	Mradi wa kukabiliana na malaria-GLOBAL FUND	9,141,000.00
9	Mradi wa chanjo wa watoto chini ya miaka mitano-GAVI	138,000,000.00
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>5,473,962,000.00</b>
	<b>Jumla Kuu ya fedha za miradi ya maendeleo</b>	<b>12,723,836,139.00</b>